




# MUONGOZO WA IBADA YA UMRAH NA HAJJ

.

MIIQAT




Miongoni mwa mambo muhimu kwa wenye kuhiji au kufanya 'Umra ni kufahamu vituo ambapo watanuia kuanza kuhiji rasmi na kuvalia vazi la Ihram. Vituo hivi huitwa Miiqaat. Miiqaat ni vituo maalum vilivyowekwa katika njia za sehemu mbali mbali za kuingilia sehemu takatifu (Haram) ya Makka ambapo mahujaji wakifika humo huvua nguo zao za kawaida na kuvalia vazi rasmi la Ihram na kunuia rasmi kuanza ibada ya Hija au 'Umra. Vituo vya kunuia Hijja alivyoviweka Mtume (s.a.w) kwa watu wa kutoka kila upande ni hivi vifuatavyo:

Haifai kwa anyetakag kuhiji au kufanya Umra azipite sehemu hizo isipokuwa awe amehirimia. Nazo ni sehemu tano

## 1. Dhul Hulaifah

Nayo ipo upande wa kusini wa mji wa Mtume wa Madina, na unaitwa «Abyaar ‹Ali». Iko mbali na Makka kwa masafa ya kilimita 420.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Madina.



Dhul Hulaifah

## 2. Juhfah:

Nayo iko karibu ya mji wa Raabigh, na ina umbali wa kiasi cha kilomita 186 kutoka Makka.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Shaam, Masri na nchi za upande wa maghribi



Juhfah

## 3. Yalamlam:

Nayo ni bonde kubwa kwenye njia ya watu wa Yaman kwenda Makka.
Kwasasa inaitwa: Assa›diyyah, na iko mbali na Makka kwa kiasi cha kilomita 120.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Yaman.



Yalamlam

## 4. Qarnul Manaazil:

Na sasa inaitwa ( Assaylul Kabiir), na iko mbali na Makka kwa kiasi cha kilomita 75.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Najd na Twaif. Na juu yake, kwenye njia ya Twaif upande wa Hadaa kuna mahali panapoitwa Waadii Muharram.
Na pote pawili ni sehemu ya kuhirimia watu wa Najd na wale wanaokuja kupitia njia ya Twaif.



Qarnul Manaazil

### 5. Dhaatu ‹Irq:

na sasa inaitwa ( Dhariibah au Khuraibaat). Napo ni mahali upande wa Mashariki ya Makka. Umbali wake na Makka ni kiasi cha kilomita 100. Na kwa sasa hapo mahali pamehamwa.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa upande wa Mashariki (Iraki, Irani na nchi za nyuma yake. Na dalili ya yaliyopita ni ni riwaya iliyopokewa kutoka kwa Ibnu Abbas t kuwa alisema:
Ama Dhaatu ‘Irq haikutajwa kwenye hadithi iliyotangulia, na lililowekwa ni ‘Umar ibnu l-Khattaab [Imepokewa na Bukhari.].



Dhaatu ‹Irq



## Maelezo

- Mwenye kuvuka sehemu hizi za mikati bila ya kuhirimia ni lazima kurudi na kuhirimia ikiwezakana, na isipoweza kufanya hivyo basi atawajibika kutoa fidiya, nao ni mbuzi atakae mchinja makka na agawanye nyama yake kwa masikini wa makka.
- Mwenye kupita sehemu za Mikaati kwa mtu asie kuwa ni wasehemu hiyo basi atahirimi hapo, lau mtu wakutoka najdi amekuja kwa njia ya watu wa madina atahirimia sehemu ya watu wa madina (Abyaar Ali)
- Mtu ikiwa nymba yake iko ndani ya sehemu ya kuhirimia kwa upande wa makka basi Mtu huyu atahirimia hija na umra sehemu alipo Mfano wa watu wa Jiddah na Bahra na Ashraa'i.
- Mwenye kuja kwa njia ya anga na bara, na bahari, huyu atahirimia akiwamkabala na sehemu ya Mikati iliyo karibu. Kwa kauli ya umar binl-

khatwab (angaliyani mkabala wake kutoka kwenye njia yenu) [Imepokewa na Bukhari.]

- Mwenye kutia nia ya kuhiji kwa mtu wa makka au asie kuwa mtu wa makka huyu atahirimia makka, ama akitaka kufanya Umra atatoka kwenda tan'iim na Ji'iraan nazo ni sehemu ziko nje ya mipaka ya haram

## NAMNA YA KUFANYA UMRAH

1. Atakayefanya Umra afikapo mahali pa kuhirimia, ataoga, atavaa mavazi ya kuhirimia





Atanuia Umrah hali ya kusema:

[لبيك عُمْرَة]

[Tunakuitikia kwa ibada ya Umra].

2. Ataanza kuleta Talbiya (Labeka), Sheria imeweka aseme:

[لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْك، لَبَّيْك لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ، لَا شَرِيكَ لَكَ]

[Tunakuitikia kwa ibada ya Umra.tumekuitikia! Sifa njema na neema ni zako na ufalme! Huna mshirika!]
[Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

Na ataendelea kuleta Labeka mpaka aione Alkaba na alisalimie Jiwe Leusi. Akifika Alkaaba atawacha Talbiya.

3. Atakwenda aingie Msikiti wa Haram, aanze kwa mguu wake wa kulia na aombe dua ya kuingia msikitini.


بسم الله ، والصلاة والسلام على رسول الله ، اللهم اغفر لي ذنوبي ، وافتح لي أبواب رحمتك ، أعوذ بالله العظيم ، وبوجهه الكريم ، وبسلطانه القديم من الشيطان الرجيم،



**Twawwaaf:**


Ni kuzunguka mara saba kuanzia Hajarul-Aswad (jiwe jeusi) na kuanza kwa kusema:

بسم الله والله أكبر




## Bismillahi Wa-Allaahu Akbar

Unapozunguza Twawwaaf, unaweza kusoma Qur-aan au kumtukuza Allaah (Subhaanahu wa Ta'aalaa) yaani Subhaana Allaah, au Kumshukuru, yaani Alhmadulillah, au Tahliyl yaani Laa Ilaah Illa Allah, au kuleta takbiyr yaani Allaahu Akbar, au kumswalia Nabiy (Swallah Allahu 'alayhi wa aalihi wa sallam), au kusoma duaa zozote unazotaka. Lakini sio kusoma vile vitabu ambavyo vinauzwa na vimeandikwa duaa za kila Twawwaaf na du’aa yake, vitabu hivyo vimeandikwa na watu na havina ushahidi kutoka




katika Hadiyth za Nabiy kuwa alifundisha du’aa hizo zilizopangiliwa kwenye hivyo vitabu, bali ni mambo ya uzushi na juu ya hivyo yanasababisha zahma za watu kwa kutembea pole pole huku wakisoma vitabu kwa sauti. Ni bora kusoma du’aa zako mwenyewe unazohitajia kwa matatizo yako na shida zako, kwani hiyo ni fursa ya kuomba kila unachokitaka na kutamani kuliko kusoma vitabu hivyo ambavyo wengi hawajui hata maana ya yaliyoandikwa ndani yake.

Na kila unapofika katika Rukn (nguzo) ya Yamani hadi katika jiwe jeusi unasema:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

((Rabbanaa Aatinaa Fid-Duniyaa Hasanataw-Wafil-Aakhirati Hasanataw-Waqinaa 'Adhaaban-Naar)).

"Rabb wetu Mlezi, Tupe duniani mema, na Aakhirah mema, na Utulinde na adhabu ya Moto"


Ukifika katika Hajarul-Aswad (jiwe jeusi) utaashiria kwa mkono wako kuelekea jiwe hilo na kusema

بسم الله و الله أكبر

Bismillahi Wa-Allaahu Akbar

Utakuwa umemaliza Twawwaaf moja. Utaendelea hivyo hadi umalize Twawwaaf (mizunguko) zote saba.

Haifai kujilazimisha kwenda kuligusa au kulibusu Hajarul-Aswad na kusababaisha zahma na kusongamana zaidi na watu kwani inatosheleza




kuashiria kwa mkono na thawabu ni zile zile, bali pengine ni zaidi kuliko mwenye kusababisha kusukumana na wenzake kwa ajili ya kutaka kuligusa jiwe.

## Rakaa Mbili Katika Maqaamu Ibrahiym




Ukimaliza Twawwaaf ya saba utasogea upande wa Maqaamu Ibraahiym na utaswali Rakaa mbili, Rakaa ya kwanza utasoma Suwrah Al-Kaafiruun (Qul Yaa Ayyuhal-Kaafiruun) na ya pili utasoma Suwral Al-Ikhlaasw *(*Qul-Huwa Allahu Ahad*)*.

Kwa hali ilivyo hivi sasa sehemu hiyo imekuwa ni zahma sana, hivyo haikupasi kujilizamisha kuswali karibu kabisa na Maqaamu Ibraahiym, bali unaweza kusogea mbali kabisa almuradi umeelekea hiyo Maqaam ya Ibraahiym. Ni makosa kusababisha zahma zaidi na msongamano na kuswali sehemu ambazo zina zahma kuzidi kuleta mashaka kwa Waislamu wengine

## Sa'y


Utakwenda Swafaa na kuanza Sa’y kwa kupanda juu ya kilima cha Swafaa na utaelekea Kaaba na kusema:



لا إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ وهُوَ عَلَى كُلِّ شَيءٍ قَدِيرٌ، لا إِلَهَ إِلا اللهُ وَحْدَهُ أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ وَهَزَمَ الأَحْزَابَ وَحْدَهُ

Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu Laa Shariyka Lah, Lahul-Mulku Walahul-Hamd Wa Huwa 'Alaa Kulli Shay-in Qadiyr. Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu, Anjaza Wa'dahu Wanaswara 'Abdahu Wahazamal-Ahzaaba Wahdahu))

"Hapana Rabb Apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah, hali ya kuwa peke Yake, wala Hana mshirika Wake, ni Wake Ufalme na ni Zake sifa njema. Naye juu ya kila kitu ni Muweza. Hapana Rabb apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah hali ya kuwa peke Yake, Ametekeleza ahadi Yake, na Amemnusuru mja Wake, na Amevishinda vikosi peke Yake"



Utaomba du’aa zako unazotaka kisha utaanza Sa’y ukifika Marwa utakuwa umemaliza Sa’y moja, utapanda kilima na kusema hivyo hivyo na kuomba kwa kuelekea vile vile Ka’abah. Kuanzia Swafaa na kufika Marwa unahesabu kuwa ni moja, na kutoka Marwa na kufika tena Swafaa ni mbili hivyo hivyo hadi utamalizia Sa’y yako ya saba katika kilima cha Marwa.



Ufikapo marwa elekea kibla ulete dua kama ulivyofanya katika swafaa.







Kama ni mwanamme atanyoa au kupunguza nywele, na mwanamke atakata tu kidogo nywele zake kama inchi moja hivi au chini yake.

# HAJJ

## NGUZO ZA HIJJAH

Ibada ya hijjah ina nguzo ambazo kama hujazitekeleza hijjah yako haiwezi kusihi. Nazo ni:

1 Kuhirimia katika vituo vya kuhirimia (Miiqat)

2-Kusimama Arafah

3-Tawaful-Ifadhah (Tawafu ya Nguzo)

4- Kusai kati ya safa na marwa.

## MAMBO YA WAJIBU KATIKA HIJJAH

1- Kuhirimia katika vituo vya kuhirimia hijjah.
2- Kusimama Arafah mpaka kuzama kwa jua.
3- Kulala muzdalifah, kisha kuondoka hapo baada ya nusu ya usiku. Ilio bora mahujaji wanatakiwa kuondoka hapo muzdalifah baada ya salatul fajri , isipokua kwa wanawake na watu wenye dharura kama watu wazima na wanaowasaidia.Wanaweza kuanza kuondoka kuanzia saa kumi alfajiri.
4- Kulala minaa kuanzia tarehe 10-12 dhulhijjah kisha kuondoka na kwenda kulala makkah na hili liwe kabla ya kuzama kwa jua. Ikiwa jua litazama na bado upo hapo minaa utalazimika kulala na kwenda kutupa mawe tarehe 13 kisha kuondoka kuelekea makkah.
5- Kurembea maguzo matatu kunatakiwa kuwe kwa kufuata utaratibu alioufundisha mtume wetu Rahma na Amani iwe juu yake.

6- Kunyoa au kupunguza na kunyoa kwa wanaume ni bora zaidi na kwa wanawake watapunguza kidogo tu nywele zao.
7- Tawaafu ya kuaga kwa wanaume na wanawake ambao hawamo katika ada zao za kike.
Ni makosa kuacha moja kati ya hayo mambo ya wajibu. Atakae acha moja kati ya hayo itamlazimu achinje mnyama na hijjah yake itakua sahihi.

AINA YA IBADA ZA HIJJAH.
1- Tamattu-Hapa hajj ahirimie umrah katika miezi ya hijjah mpaka amalize na ajitoe kwenye ihram. Na katika mwaka huohuo ahirimie tena kwa ajili ya hijjah. Mwenye kufanya tamattu akifika Makkah atafanya amali za umrah ambayo ni:kutufu,kusai kisha kunyoa au kupunguza nywele. Kisha atajitoa kwenye ihramu zake. Ikifika tarehe nane mwezi wa hijjah atavaa ihramu na atafanya amali za hijjah na atalazimika kuchinja kwa kupumzika kwake.
2- Qiraan- Hajj atahirimia hijjah na umrah kwa pamoja, au ahirimie umrah kisha anuilie

kufanya hijjah kabla ya kuanza kufanya tawafu , na mwenye kufanya Qiraan atabaki kwenye ihramu yake mpaka amalize kufanya hijjah, na atalazimika kuchinja kwa kule kuhirimia pamoja kwa amali ya hijjah na umrah.
3-Ifraad -Hajj ahirimie hijjah peke yake na mwenye kufanya ifradi atabaki na ihramu zake mpaka amalize kuhiji na haitomlazimu kuchinja.

## ULETAJI TALBIYA NA SEHEMU ZAKE.

Baada ya kuhirimia katika miiqat, utaanza kuleta Talbiya kwa wingi ukiwa njiani kuelekea makkah.
Na inatiliwa mkazo mahali pengi kama:
Ukipanada sehemu zilizoinuka juu au ukiteremka kwenye bonde ,au baada ya kuswali sala za faradhi,au ukaingia usiku au mchana.
Unaacha kuleta talbiya ukiwa kwenye umrah unapoiona alkaaba na ukiwa kwenye hijjah utakapoanza kurembea kiguzo cha mwisho siku ya idd.

# MATENDO KATIKA SIKU ZA HIJJAH

## MATENDO YA SIKU YA 1 TAREHE 8 DHULHIJJAH(SIKU YA TARWIYAH)

Kuhirimia na kuleta nia ya kuingia katika ibada ya hijjah.

Haji atahirimia kwa ajili ya Hijjah kwa kusema اللهم لبيك حجا

Kisha ataanza talbiya kwa kusema

[لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ، لاَ شَرِيكَ لَكَ]

Wanaume peke yao wataleta kwa sauti kubwa na wanawake kwa sauti ndogo.

Elekea mina na huko utaswali swala za faradhi kwa kufupisha rakaa nne ziwe rakaa mbili mbili kwa wakati wake.

Utalala mina na utaswali hapo sala ya Alfajiri.

## MATENDO YA SIKU YA 2 TAREHE 9 DHULHIJJAH(SIKU YA ARAFA)

Baada ya kuchomoza jua utaelekea Arafa huku unaleta talbiya kwa wingi.

Utaswali Arafa swala za Adhuhuri na Alasiri kwa kufupisha rakaa mbilimbili.Itakua na adhana moja na Iqama mbili.

Jitahidi kuzidisha dua na nyiradi huku unaelekea qibla. Nyanyua mikono yako juu uombe dua mpaka kuzama jua.

Uradi bora zaidi siku hii maalum ya arafa iliothibiti katika sunnah ni kusema:

لا إله إلا الله وحده لا شريك له ، له الملك ، وله الحمد ، وهو على كل شيء قدير



## *USIKU WA SIKU YA KUMI UTALALA MUZDALIFA*

Jua litakapo zama, haji ataanza safari ya kuelekea Muzdalifa na huko ataswali kwa kufupisha kwanza sala ya magharibi rakaa tatu kama kawaida kisha rakaa mbili ya sala ya Isha.

Kabla ya kulala utatafuta vijiwe saba vidogo ya kwenda kurembea kesho yake Jamaratul Aqaba. Okota vijiwe saba peke yake kwa ajili ya kutupa kwenye jamarati,ama masiku yanayobaki utaokota vijiwe mina au sehemu yoyote.



Utalala hapo na Utaswali alfajiri hapo. Baada ya alfajiri inapendekeza kuelekea kibla na kuzidisha dhikri na dua hali ya kua umeinua mkono wako na uendelee hivyo mpaka kupambazuke sana. utaendelea na dua na nyiradi kwa wingi.

Kabla ya jua kuchomoza utaelekea mina.




## SIKU ZA TASHRIIQ AREHE 10,11,12,na13

Masiku ya Tashriiq ni masiku tatu.Siku ya 10,11,12 na 13. Zimeitwa kwa jina hilo kwa sababu nyama za udh-hiya zikikatwakatwa na kuanikwa juani ili zikauke na Mtume rehma na amani zimuendee amesema kua masiku haya ni masiku ya kula na kunywa na kumtaja Allah alietukuka.

## MATENDO YA SIKU YA 3 YA SIKU YA IDDI 10 DHULHIJJAH

Elekea mina kabla jua halija chomoza.

Ufikapo mina,elekea katika Jamaratul Aqaba ulirembee vile vijiwe saba ulivyookota usiku wa muzdalifa huku unaleta takbira kila unaporembea kwa kusema:

الله أكبر



Baada ya kurembea utachinja mnyama ukiwa utaweza na usipoweza basi makampuni ya kuchinja watakuchijia.




Baada ya hapo utanyoa na kupunguza nywele na kunyoa ni bora zaidi kwa wanaume.







Hapa utakua umemaliza hatua ya kwanza ya hijjah (tahalul Al awwal). Hapa utatoa Ihramu yako na kuvaa mavazi yako ya kawaida na pia ukitaka unaweza kujitia manukato mazuri.Hapa utakua umehalalikiwa kila kitu ila tu mke wako huwezi fanya nae tendo la ndoa.

Utaelekea makkah(Alkaabah) kufanya tawaful ifadhah.

Baada ya hapo utafanya sai ikiwa unafanya hajj ya tamattui. Pia ikiwa hufanyi hijjah ya tamattui na hukufanya tawaful quduum.

Kufikia hapa utakua umefanya tahalul ya pili na utahalalikiwa kila kitu hata mkeo.Baada

ya hatua zote hizo utarudi minaa na kuendelea kulala huko.

## MATENDO YA SIKU YA 4 TAREHE 11 DHULHIJJAH

Rembea maguzo yote matatu mawe saba.

Lala minaa mpaka tarehe 12 Dhulhijjah.

## MATENDO YA SIKU YA 5 TAREHE 12 DHULHIJJAH

Rembea majiwe yote matatu kama ulivyo fanya siku ya nne.

Ukitaka kuondoka minaa tarehe 12 dhulhijjah itakulazimu uondoke kabla ya jua kuzama lakini baada ya kurembea maguzo yote matatu. Na ukiamua kulala utarudi minaa katika mahema.

## MATENDO YA SIKU YA 6 TAREHE 13 DHULHIJJAH.

Rembea maguzo yote matatu kama ulivyo fanya hapo nyuma.



Utaondoka minaa.

Tendo la mwisho ni tawaful widaa (tawafu ya kuaga).

Tawafu ya kuaga ndio kitu cha mwisho utakachokifanya katika nyumba tukufu.



“Mmoja wenu asiondoke mpaka iwe sehemu yake ya mwisho ni katika nyumba ya Allah”

## MJI WA MADINA NA JINSI YA KUUZURU MSIKITI WA MTUME REHMA NA AMANI ZIMWENDEE



Mji wa Madina ndipo mahala alipohamia Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee, na hapo ndipo alipozikwa.

Katika mji huo upo Msikiti wa Mtume , ambao ni moja kati ya Misikiti mitatu mitukufu ambayo haruhusiwi mtu kuifungia safari ispokuwa miskiti hiyo,kama alivosema Mtume- rehma na amani zimwendee- kwamba: « Haifungwi safari ya kiibada ispokuwa kuielekea miskiti mitatu:
Almasjed Alharam
Wal Masjed Alaqsa
Pamoja na kuwa kuuzuru Msikiti wa Mtume sio wajibu wala sharti katika Hijjah,bali pia hakuna mafungamano wala mahusiano yoyote,wala ziara hii haina Ihraamu,ispokuwa ni jambo ambalo linatambulika kisharia,na linapendeza kwa muda wowote ndani ya mwaka.
Kwahiyo pindi Allah anapomuwafikisha mja,na akamrahisishia kufika katika nchi hii yenye Haramu mbili tukufu basi inakuwa ni Sunna kwake kwenda Madina,ili akaswali katika Msikiti wa Mtume -rehma na amani za Allah zimwendee-,maana kuswali katika msikiti huu swalainakuwa ni bora kuliko kuswali swala elfu moja katika miskiti mingine,ispokuwa Msikiti Mtukufu wa

Makkah. Na Msikiti wangu huu (yaani msikiti wa Madina)
Maana swala katika Msikiti Mtukufu wa Makkah inakua ni sawa na swala laki moja katika miskiti mingine.




Wakati wa kuingia msikitini atatanguliza mguu wa kulia na huku akisema :

بسم الله والصلاة والسلام على رسول الله ، أعوذ بالله العظيم وبوجهه الكريم وبسلطانه القديم من الشيطان الرجيم، اللهم افتح لي ابواب رحمتك

Dua hii pia yatakiwa isomwe wakati wa kuingia katika miskiti mingine.
Na baada ya kuingia kwake msikiti wa Mtume ataanza kwa kuswali rakaa mbili za maamkizi ya msikiti,na itapendeza sana kama ataziswali mahala panapoitwa Arraudhwa (ambalo ni eneo lilipo baina ya kaburi ya Mtume na mimbari yake),



Lakini kama hakuweza basi ataswali sehemu yoyote ile hapo msikitini,kisha ataelekea katika kaburi ya Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee- asimame mbele yake hali ya kuielekea, aanze kumsalimia kwa adabu na kwa sauti ya chini, aseme hivi :



(Assalaamu alayka ayyuhan-nabiyyu warahmatullahi wabarakaatuh),
kisha amswalie.
Nakama atasema: Ewe Allah mpe njia na fadhila,na umfufue katika daraja ulilomuahidi,Ewe Allah mpe malipo ya kuutumikia Ummah wake malipo yaliyokuwa bora. Akisema hivyo sio vibaya.

Kisha anageuka...
upande wa kulia kidogo ili asimame mbele ya kaburi la Abu- ubakaris-siddiiq- Radhi za Allah zimwendee- atamsalimia na kumuombea rahma na msamaha na radhi.
Kisha anageuka...
kidogo tena kuliani kwake,ili asimame mbele ya kaburi la Umar Ibnil-khatwaab -Radhi za Allah zimwendee- atamsalimia na ku-muombea rahma na msamaha na radhi.
Na imegundulika kwamba..
baadhi ya watu wanao uzuru Msikiti wa Mtume- Rehma na amani zimwendee- wanafanya makosa ambayo yanazingatiwa ni miongoni mwa uzushi ambao hauna asili

katika Dini,wala ha- ukupokewa kwa Maswahaba .
Na miongoni mwa makosa hayo ni kama haya yafuatayo....
Kujipangusa katika vyuma vilivyo katika chumba hicho na kuta za msikiti.
Kulielekea kaburi wakati wa kuomba dua.
Na usahihi ni kuelekea Qibla wakati wa kuomba dua .



Kuyazuru makaburi ya watu wa Baqii ambayo wamezikwa Maswahaba wengi sana hapo,ikiwa miongoni mwao ni Khalifa watatu Uthmani -Radhi za Allah zimwendee .


Kuyazuru makaburi ya Mashahidi wa vita vya Uhudi,na miongoni mwaao ni yule bwana wa Mashuhadaa wote ambaye ni Hamza bin Abdil mutwalibi -Radhi za Allah ziwaendee -awasalimie na kuwaombea dua kama ambavyo Mtume – Rehma na amani za Allah zimwendee- alivyowafundisha Maswahaba wakati wa kuzuru makaburi :
Aondoke hali akiwa na twahara kwenda katika Msikiti wa Qubaa,ambao ndio Msikiti wa kwanza uliojengwa katika Uislamu,ili akauzuru na apate kuswali humo,kama alivyofanya Mtume mwenyewe na akawahimiza katika hilo ,kama anavyo sema Sahal bin Saad-Radhi za Allah zimwendee- kwamba Mtume -Rehma na amani za Allah zimwendee amesema:
« من تطهر في بيته ثم اأتى مسجد قباء فسلى فيه سلاة كان له كاأجر عمرة »
«Mwenye kujitwaharisha nyumbani kwake,kisha akaelekea katika Msikiti wa Qubaa na akaswali katika Msikiti huo, hupata ujira wa Ibada ya Umrah».

Pia imekuja katika swahihi mbili (Bukhari na Muslim) katika Hadithi ya Abdallah Bin Umar- Radhi za Allah ziwaendee-amesema: « Mtume -Rehma na amani zimwendee- alikuwa akiuzuru Msikiti wa Qubaa kwa kipandwa au kwa miguu,na anaswali rakaa mbili.



Baada ya Msikiti huu hapo Madina hakuna Miskiti mingine wala maeneo mengine

ambayo sharia imetutaka tuyazuru illa baitul maqdis ambayo ipo palestina.




DAAWA KWA NJIA
YA MTANDAO